

102/3  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
JULAI / AGOSTI 2014  
MUDA:  $2\frac{1}{2}$

**MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA  
NANDI KASKAZINI 2014**  
**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA KIDATO CHA NNE**

KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
MUDA:  $2\frac{1}{2}$

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Fasihi simulizi na Hadithi Fupi
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
5. Karatasi hii ina kurasa nne. Watahini ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

- 1) Kenya ewe Kenya  
U nchi tukufu  
Umepambwa kwa marefu  
Lakini u kipofu!  
Kwa nini?
- 2) Mkoloni alikunyanya  
Kwa madhi la ukapitika  
Mzalendo niliteseka  
Mwisho ukafika!
- 3) Sitini na tatu  
Uhuru wetu  
Tulipata  
Tukafurahiya  
Tulidhani ameenda mkoloni!
- 4) Miaka hamsini baadaye  
Hatujapata uhuru, hatimaye  
Tungali minyororoni  
Mwa weusi wakoloni!
- 5) Tatalia hadi lini?  
Majanga kwetu kawaida  
Si mafuriko si kiangazi  
Twafa ja nzi  
Hasa kaskazini ya nchi!
- 6) Ufisadi umezidini  
Ofisini na mitaani  
Trafiki nao barabarani  
Sadaka huchukueni!
- 7) Nyumba ya Mungu si salama  
Kasisi mewa fisi  
Watoto huwanajisi  
Ukware umeshika kasi  
Maombi hulipiwa fisi!
- 8) Kenya si salama  
Raiya tunahama  
Makaidi wana hujuma  
Watu wauwawa  
Kumbuka westgate!
- 9) Maskini wanaumiya  
Chakula mepoteya  
Garama mezidiya  
Tajiri hufurahiya  
Mishahara minono hupokeya  
Magari makubwa hutumiya!

10) Tungoje miaka mia moja?

Ndipo tuwe  
Wenye umoja?  
Lini tutajivunia  
Kuwa wakenya?  
Tumevumilia  
Kuwa wakenya!

### **MASWALI**

- (a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
- (b) Utunzihuu ni wa kishairi. Toa sifa za kishairi zinazojitokeza. (alama 2)
- (c) Ni tamathali zipi za usemi zilizotumiwa katika shairi hili? (alama 4)
- (d) Taja nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
- (e) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)
- (f) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa saba. (alama 3)
- (g) Eleza umbo la shairi hili. (alama 3)
- (h) Eleza maana ya mafungu yafuatayo yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
- (i) Makaidi wana hujuma.
- (ii) Kwa madhila ukapitika.

### **SEHEMU YA B: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**

#### **Jibu swali la 2 au 3**

2. "Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi?"

- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- (b) Anayerejelewa kuwa mwendawazimu katika dondo hili ni mwendawazimu asiyenawazimu. Thibitisha kauli hii ukizingatia Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

- (c) Eleza sifa za mzungumzaji katika dondo hili. (alama 6)

3. Kidagaa Kimemwozea ni Riwaya inayosawiri uozo katika jamii ya sasa. Jadili.

(alama 20)

### **SEHEMU C: TAMTHILIA**

#### **MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)**

#### **Jibu swali la 4 au 5**

4. Maisha ya viongozi wa Cheneo na marafiki wao yalikuwa bora zaidi ukilinganisha na watawaliwa. Fafanua. (alama 20)

5. "Wafanyakazi katika bohari ya maruta wamegoma."
- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- (b) Toa sababu nne kwa nini wafanyakazi wanagoma kulingana na muktadha huu. (alama 4)
- (c) Wafanyakazi walifanya kazi kwa masaibu mengi kule Cheneo. Fafanua. (alama 12)

#### **SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI**

- 6.
- (a) Ngomezi ni nini? (alama 2)
- (b) Bainisha sifa nne za ngomezi. (alama 4)
- (c) Eleza majukumu manne ya ngomezi katika jamii. (alama 8)
- (d) Ni vizingiti gani vinavyoweza kuathiri matumizi ya ngomezi siku hizi? (alama 4)
- (e) Vianzo vya ngano vina majukumu gani? (alama 2)

#### **SEHEMU E: HADITHI FUPI**

##### **DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

##### **Jibu swali la 7 au la 8**

7. "Nashangaa vile kwetu tunavyowaabudu watu hao wasiotujali."  
"Kwenu wapi?"  
.....
- "Ahaa! You guys are our brothers",
- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- (b) Eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika dondo hili. (alama 2)
- (c) Jadili sifa zozote **tatu** za msemaji na tatu za msemewa. (alama 12)
8. Jadili maudhui ya tamaa katika, "Samaki wa Nchi za Joto na Doreen Baingana. (alama 20)